



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI
SHIRIKA LA POSTA TANZANIA



Shindano la Kimataifa la Uandishi wa Barua kwa Wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari.

 **2 Februari - 22 Aprili 2025**



Shirika la Posta Tanzania linafuraha kuwaalika wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari hapa nchini kushiriki Shindano la 54 la Kimataifa la Uandishi wa Barua linaloratibiwa na Umoja wa Posta Duniani (UPU) kwa mwaka 2025.

01

MADA

“Fikiria wewe ni bahari. Mwandikie mtu barua ukimwelezea kwa nini na kwa namna gani wanapaswa kukutunza vizuri.”

02

UREFU

Barua iandikwe kwa mkono yenye maneno yasiyozidi 800; inapaswa kuwa barua na sio insha.

03

SIFA YA UMRI

Mshiriki awe na umri kati ya miaka 9 hadi 15

04

LUGHA

Wanafunzi wa shule za Msingi wanaweza kuandika kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza, ila wanafunzi wa shule za Sekondari wanapaswa kutumia lugha ya Kiingereza pekee.



ZAWADI

Washindi watatu wa kwanza watapata zawadi mbalimbali, zikiwemo fedha taslimu na vyeti.

Barua ya mshindi wa kwanza wa Kitaifa itawasilishwa Makao Makuu ya Umoja wa Posta Duniani Berne - Uswizi, ambako itaiwakilisha Tanzania katika Shindano la Kimataifa la Uandishi wa Barua. Umoja wa Posta Duniani utatoa tuzo maalumu za Medali na Vyeti (Medali ya Dhahabu kwa mshindi wa Kwanza, Medali ya Fedha kwa mshindi wa Pili na Medali ya Shaba kwa mshindi wa Tatu). Mshindi wa Medali ya Dhahabu atagharamiwa safari ya kwenda Makao Makuu ya Umoja wa Posta Duniani ambako atakabidhiwa zawadi.



MUHIMU

Barua inapaswa kujumuisha jina kamili na anwani ya mshiriki, umri na tarehe kamili ya kuzaliwa, jinsia (kiume/kike), na Jina la Shule/ Taasisi anaposoma, pamoja na kubandika stempu sahihi na kutuma kupitia ofisi ya Posta kabla ya tarehe 22 Aprili, 2025, kwa anwani ifuatayo;



Mkurugenzi wa Masoko na Mauzo,
Shirika la Posta Tanzania,
Jengo la Posta,
7 Mtaa wa Ghana,
S.L.P 9551,
11300 DAR-ES-SALAAM.

ANGALIZO;

Washiriki wanapaswa kuandika barua kwa rafiki au mtu mwingine, si kwa Shirika la Posta Tanzania. Kila barua inapaswa kuwekwa katika bahasha yake iliyobandikwa Stempu. Kutuma barua zaidi ya moja katika bahasha moja ni kinyume na utaratibu, hivyo mshiriki atakayekiuka utaratibu huu, ataenguliwa katika mashindano.